BIBLIA KWA TASWIRA, AGANO LA KALE, KITABU CHA 20
1 SAMWELI, Sehemu ya Kwanza

U A S I

(VISUALIZED BIBLE, Vol 20, OT, Disobedience)
Mwandishi: Arlene S. Piepgrass
Muchapaji: Todd Tennant
Imegeuzwa kwa Swahili Congo na watumishi wa Mungu katika DR Congo

© Bible Visuals International
PO Box 153, Akron, PA 17501-0153
Simu: 717-859-1131
www.biblevisuals.org

SOMO 1 - UASI KATIKA JAMAA.

Kwa mwalimu kujifunza mbele: 1 Samweli 1:1 hadi 3:21

Shabaa ya somo: Kuonyesha kama Mungu anaazibu uasi katika jamaa.
Yale ambayo wanafunzi wako wangelipaswa kujua: Kwamba sababu Mungu ni mwema, Anafundisha wababa kwadibisha watoto wao.
Yale ambayo wanafunzi wako wangelipaswa kutambua: Wenye shukrani kwa wazazi wanaofundisha matokeo mazito ya kufanya zambi mbele ya Mungu.
Yale ambayo wanafunzi wako wangelipaswa kufanya: Wale wanaoendelea kulindwa na wazazi – watii wazazi wao; washike maongozi yao. Wale wanaokuwa wazazi – wakazane na watoto wao, halafu wataweza kwa kutaka kwao kumutii Mungu.

Somo kwa kifupi: (kuandika ndani ya buku ya mwalimu na za wanafunzi.)
1. Kosa la Eli katika jamaa lake.(2 Samweli 2:12-17, 22-25).
2. Mungu anatupilia mbali jamaa la Eli.(1 Samweli 2:27-36).
3. Utii wa Elekana na Hana. (1 Samweli 1:1 hadi 2:11, 18-21).
4. Mungu anachagua Samweli.(1 Samweli 2:35 hadi 3:21).

Shairi la kujua kwa ufahamu: "Mwogope Bwana tu, mumutumikie kweli kweli kwa mioyo yenu yote; maana kumbukeni mambo makubwa gani aliyowatendea ninyi." 1 Samweli 12:24.

Utangulizi: Maelezo kwa mwalimu:

Kwa muda wa miaka 100 iliyotangulia wakati wa kitabu cha kwanza cha Samweli, watu wa Israeli walimuasi Mungu mara kwa mara. Zaidi kuliko kumwabudu, walitumikia miungu ya uwongo ya Wakanana. Hawakutii amri ya Mungu ya kuangamiza mataifa jirani ya wapagani. Kwa hiyo walishindwa na kutawaliwa na mataifa yale. Wakati Waisraeli walitubu kwa kweli zambi yao na kuomba Mungu awasamehe, Alisikia maombi yao. Kila wakati alisimamisha kiongozi mwenye nguvu – aliyeitwa mwaamuzi – kuwaokoa toka waadui zao. Kitabu cha Waamuzi katika Biblia kinaeleza mambo ya wakati uliopita ya Israeli.

Kitabu cha Samweli wa kwanza kinaendelea na historia ya watu wa Israeli. Samweli aliishi wakati Samusoni alipokuwa akiishi naye alimugomboa sawa vile mwamuzi wa Israeli. Kwa wakati huu, Waisraeli walikuwa wanatendewa kwa ukali na waadui zao, Wafilistini.

Mafundisho ya kihistoria toka Biblia inaeleza habari za nguvu ya zambi na matokeo yake. Mazito kwa wote wakati azabu inakosekana. Machukizo ya Mungu kwa ajili ya zambi na malipizi Yake juu ya zambi, ni onyo kwetu leo (Waebrania 10:11; Waroma 15:4; 6:23).

Somo:

1. Kosa la Eli katika jamaa lake (1 Samweli 2:12-17, 22-25.)

Eli alikuwa mutu mukubwa – kwa kweli, mutu mukubwa zaidi katika inchi ya Israeli: Alikuwa Kuhani Mukubwa, yule aliyesema na Mungu kwa ajili ya watu. Aliwafundisha watu amri za Mungu. Alieleza umuhimu kabisa wa kutii Bwana. Aliongoza Waisraeli katika maabudu yao kwa Mungu.

Ni Kuhani Mukubwa peke yake ndiye aliweza kuingia katika Pahali Patakatifu Sana (Patakatifu pa Patakatifu) katika Hema ya Kusanyiko. Na alipaswa kuingia mara moja tu kwa mwaka – Siku ya Upatanisho. Kwa siku hiyo alitwaa damu ya nyama wa sadaka kwa kuinyunyiza juu ya Sanduku la Agano. Mungu alipoona damu Alisamehe zambi za Kuhani Mukubwa na za Waisraeli wote. (Angalia Walawi 16).

Eli alikuwa na wana wawili, Hofuni na Finehasi. Sababu Eli alikuwa Kuhani Mukubwa, wana wake walikuwa makuhani. Ilikuwa heshima takatifu kuchaguliwa na Mungu kwa kumutumikia katika Hema ya Kusanyiko. (Angalia 1 Samweli 2:28; Kutoka 28:1; Walawi 8:1-30. Zamani mbele ya kuishi kwa Eli, Mungu alikuwa amechagua jamaa ya Haruni kutumika kama vile makuhani. Eli alikuwa muzao wa Haruni).

Ingawa hiyo, makuhani hawangeweza kuingia katika Pahali Patakatifu Sana, waliruhusiwa kuingia tu katika Pahali Patakatifu. Ndio wale waliomutolea Mungu sadaka ambazo watu walileta wakati walikuja kumwabudu. Ilikuwa upendeleo wa heshima kumutumikia Bwana kama vile Kuhani.

Miaka maelfu mbele ya haya, Mungu alikuwa ametoa maagizo kamili juu ya aina ya sadaka ambazo watu walikuwa wanaleta. Alifasiria waziwazi namna gani makuhani walipaswa kuchinja nyama na kwa ukamilifu namna sadaka ziliteketezwa kwa moto. (Angalia Walawi 6:1-38).

Mungu alisema: "Sehemu ya kila sadaka ni ya makuhani. Itakuwa chakula kwa ajili ya jamaa zao." (Angalia Walawi 7:34-35; 10:14).

Vilevile Bwana anasema: "Mbele ya kuwapa makuhani sehemu zao, munapaswa kuteketeza mafuta yanayofunika sehemu za ndani." (Angalia Walawi 3:4-5; 10:15). Makuhani wanapaswa kutakaswa (*Kuwekwa pembeni kwa ajili ya kazi)* kwa ajili Yangu. (Angalia Walawi 8:22-24). Wanapaswa kuwa tayari kusikiliza sauti Yangu, kunitumikia Mimi kwa utiifu, na kutembea katika njia Yangu. Wao ni wajumbe wa watu Wangu.

Eli alijua amri zote Mungu alizotoa. Kwa sababu hii, madaraka yake kama vile baba yalikuwa gani? (Acha wanafunzi wajibu) *Eli alipaswa kufundisha amri za Mungu kwa watoto wake).*

Hofuni na Finehasi walipaswa kufanya nini? (*Walipaswa kusikiliza na kuheshimu mafundisho ya baba yao; kumutii Mungu).* Kama Hofuni na Finehasi waliasi, walikataa kumusikiliza baba yao, na kukosa kutii Mungu, Eli alipaswa kufanya nini? *(Alipaswa kuazibu wana wake)* Biblia haituambie kama Eli alifundisha kwa uaminifu wana wake ndio ao hapana. Lakini inasema yale waliyofanya wakati walikuwa makuhani.

Onyesha taswira 1: Kila mara mutu alikuja kutoa sadaka kwa Mungu, Hofuni na Finehasi walifukuza mutumishi kwa kanya kubwa. Alichomeka kanya ndani ya chungu akisema: "Nyama yoyote itakayokuja juu ya kanya ni ya makuhani!"

Yule mwenye kuabudu, alikwa na bidii ya kutii Mungu alijibu: "Nitakupa sehemu ile ya nyama ambayo Mungu aliamuru: "Mutumishi alisema kwa ukali alikamata mingi sana kuliko alivyopaswa:" Nyama hii haitoshi.! Mutumishi akaomba: "Hapana ile tu, bwana wangu hapendi zaidi nyama yenye kuchomwa, sasa nitakupatia yenye kutokoteshwa. Sasa hivi, unipe nayo ikiwa mbili."

Yule mwenye kuabudu mwenye utii alikazania akisema: "Hapana, hapana! Mungu anatuamuru kuteketeza kwanza mafuta. Halafu unaweza kutwaa ile unayotaka."

Mutumishi akasema kwa sauti kubwa: "Utupatie, ao tutaitwaa kwa nguvu." Wale makuhani wawili, Hofuni na Finehasi walizarau sheria za Mungu, na kufanya sheria zao wenyewe. Walitia mukazo kwamba watu wamuasi Mungu. Halafu Waisraeli wakaacha kuleta sadaka.

Hofuni na Finehasi wangelipaswa kuwa wazuri, mifano ya utii kwa Mungu Mwenye uzima. Kuliko vile, walifanya makosa na maovu mengi. Waliiga hata makuhani wapagani walioabudu sanamu. (1 Samweli 2:22-23)! Walifanya maabudu ya Bwana Mungu sawasawa na maabudu ya wapagani. Biblia inaonyesha kweli kama Eli, Kuhani Mukubwa, alikuwa mwenye kujipendelea na mwenye zambi. Alipendelea sana chakula kizuri kuliko kutii maagizo ya Mungu. Alikula nyama zilizokatazwa pamoja na wana wake wote wawili (1 Samweli 2:29)

2. Mungu anatupilia mbali jamaa la Eli (1 Samweli 2:27-36.)

Kila mutu alikuwa anasema juu ya mwenendo mbaya wa Hofuni na Finehasi. Unafikiri Eli alipaswa kufanya nini? (Usukume wanafunzi wapate kuzungumuza. *Eli alipaswa kuwafukuza katika kazi ya ukuhani. Hii ndiyo malipizi waliyostahili).* Kuliko kuadibisha wana wake, Eli aliwaambia: "Ninasikia habari mbaya juu ya mwenendo wenu. Mukumbuke: Mungu atawaazibu kwa kumuasi."

Hofuni na Finehasi wakapandisha mabega yao na kugeuka toka mbele ya baba yao. Wakaendelea na uovu wao, wakikataa kumutii. Sababu Eli hakuadibisha wana wake, Bwana akatuma maonyo kwake kwa njia ya mutu wa Mungu.

Onyesha taswira 2: Yule mutu akaanza kusema: "Eli, Mungu amenipatia ujumbe wako. Unawaheshimu wana wako zaidi kuliko Mungu kwa kuwaruhusu kuasi maagizo Yake. Sababu haukuwaazibu wana wako, Mungu atawaazibu. Sababu ya uovu wao, Hofuni na Finehasi watakufa kwa siku moja. Bwana Mungu atachagua jamaa lingine kuwa makuhani – watu wanaokuwa tayari kumutii Yeye,"

Eli alisumbuka sana alipopata ujumbe huu toka kwa Mungu. Alitambua kwamba alingojea muda murefu sana kwa kuazibu Hofuni na Finehasi.

3. Utii wa Elekana na Hana (1 Samweli 1:1 hadi 2:11, 18-21.)

Sasa, acha niwaelezee habari za jamaa ya Mwisraeli mwingine. Elekana alikuwa mume. Hakuwa mutu mukubwa. Lakini alimupenda Mungu. Kila mwaka alikwenda kwenye Hema ya Kusanyiko (kule Shilo) kwa kutoa sadaka na kuabudu Bwana. Ni kule ndiko Eli, Kuhani Mukubwa, na makuhani Hofuni na Finehasi, walikotumikia Mungu.

Hana, muke wa Elekana alikwenda pamoja naye. Kwa sababu hakuwa na mutoto, alihuzunika – alihuzunika sana hata hakuweza kula. Kile alichofanya tu ni kulia. Kwa mwisho Hana akatoka ndani ya kundi na kwenda peke yake hekaluni, aliomba: "Bwana mupendwa, kama utanipatia mwana, nitakurudishia, naye apate kukutumikia katika maisha yake yote."

Eli akiwa anaikaa kwenye mulango wa Hema, aliona namna gani Hana alivyokuwa mwenye moyo wenye kuvunjika. Akamwambia: "Mungu akupatie kile unachoomba.

"Hana akafurahi! Aliamini kwamba Mungu atajibu maombi yake. Akakwenda haraka kwa mume wake, akacheka, na akaanza kula. Katika mwaka moja, Hana akapata mutoto mwanaume. Akamwita "Samweli," maana yake *aliyeombwa kwa Mungu*. Unafikiri ni kwa nini alichagua jina hili? (Acha wanafunzi wajibu). Hana hakusahau ahadi yake. Kwa kweli alipokuwa akibembeleza mutoto Samweli, kila mara alimwambia juu ya Hema ya Shilo. Alimwelezea kama Bwana Mungu ni Mutakatifu na Anachukia zambi. Alimwelezea juu ya wenye kuabudu na juu ya sadaka ambazo walitoa kwa kusamehewa zambi zao.

Hana aliweza kufasiria hivi: "Samweli, wewe ni zawadi toka kwa Mungu. Mbele ya kuzaliwa kwako, nilimwahidi Bwana kama nitakutoa Kwake. Nyuma kidogo utapata upendeleo wa kipekee. Utaishi katika Hema ya Kusanyiko ambamo utaweza kumutumikia Mungu. Fikiri juu ya ile Samweli, wewe, mwana wangu mudogo, utakuwa mutumishi wa Mungu Aliye Juu Sana. Heshima gani hii! Baba yako na mimi tunakupenda sana. Tutakukumbuka zaidi kuliko vile unaweza kujua. Lakini tutakuja kukuona kila mwaka. Tutakuombea kila siku. Hatutaweza kukusahau hata kidogo."

Unafikiri itaweza kuwa vyepesi kwa Hana kutoa mwana wake kwa Mungu? HAPANA! Alikuwa kabisa sawa na wa mama wengine - alimupenda mwana wake sana. Lakini vilevile alimupenda Mungu. Na alikusudia kutimiza ahadi yake Kwake.

Siku ikafika wakati Hana alisema: "Samweli, uko kijana, lakini ni umri wa kutosha kwangu kuweza kutimiza ahadi yangu kwa Bwana. Wakati umetimia kwetu kwa kwenda Shilo kwa kuabudu Mungu. Baba yako atatwaa sadaka itakayotolewa kwa Bwana kwa ajili ya zambi zetu. Nawe Samweli utabakia kule. Utamusaidia Eli katika Hema ya Kusanyiko. Yeye, Kuhani Mukubwa atakupatia kazi na kukufundisha namna ya kumutumikia Bwana Mungu."

Hana akafunga nguo za Samweli katika furushi ndogo. Na wote watatu wakaanza safari yao ndefu kwenda Shilo. Kule Elekana na Hana walitolea Bwana sadaka ya nyama.

Onyesha taswira 3: Halafu wakamupeleka Samweli kwa Eli. Hana akaeleza: "Samweli ni wako kwa kumuzoelesha kwa kazi ya Bwana. Mungu ndiye alinipa kijana huyu. Sasa ninatimiza ahadi yangu nami ninamuleta kwako kwa ajili ya kazi ya Mungu."

Akisha kumupa Bwana mwana wake pekee, Hana aliomba maombi ya kuvutia. Alianza hivi: "Moyo wangu unajaa furaha katika Bwana."

Umesikia yale? Hana alitoa kwa furaha kwa Mungu wa mbinguni. Unamutolea kwa njia kama hii? Hakumutolea Mungu tu sadaka ya nyama inayohitajika. Alipana mwana wake pekee. Na aliweza kuimba wimbo wa furaha. Je, unamutolea Mungu kwa furaha? (Angalia 2 Wakorinto 9:7),

Akimugeukia Samweli, Hana alisema: "Baba yako pamoja nami tunapaswa kurudia nyumbani sasa. Lakini, tutakuja kukwangalia kwa mwaka unaokuja. Samweli, nitakuletea kila mwaka koti mupya. Samweli, ninakupenda. Nitakuombea kila siku. Ninasifu kwona Mungu yuko na kazi ya kipekee kwa ajili yako. Kumbuka: Kila mara umutii Eli. Sikiliza kwa uangalifu yote anayokufundisha juu ya Bwana na juu ya maagizo Yake. Samweli aliangalia jinsi mama na baba yake walivyotoweka chini kwenye barabara ya udongo. Kisha, yeye mwenyewe aliabudu Mungu ndani ya Hema. Kwa muda wa miaka Samweli alitumika ndani ya Nyumba ya Mungu. Alikuwa mutiifu kwa Bwana na kwa Eli. (Soma kwa sauti kubwa na polepole l Samweli 2:21b na 26).

Unafikiri Bwana alifurahi na sadaka kubwa sana ya Hana? Kweli alifurahi! Halafu,. Alimubariki na wana watatu zaidi na wabinti wawili.

4. Mungu anachagua Samweli (1 Samweli 2:35 hadi 3:21.)

Siku moja usiku wakati Samweli alipokuwa na miaka 12, alikuwa analala sana katika Hema. Kwa ghafula sauti ikaita: "Samweli, Samweli."Aliruka toka kwenye kitanda chake, akakimbia mbio kwa Eli, akisema: Niko hapa – Uliniita." Eli akasema kwa upole: "Mwana wangu, sikukukwita. Rudi kwa kitanda."

Onyesha taswira 4: Haya yalitokea mara tatu. Kwa mwisho Eli alitambua kama Bwana Mungu alikuwa anamwita Samweli. Kwa hiyo alisema: "Samweli, wakati mwingine ukisikia sauti, useme hivi : 'Sema, Bwana, mutumishi Wako iko anasikia.' Fikiri juu ya hii! Bwana alitaka kusema na kijana Samweli!

Bwana aliita tena, Samweli akajibu: "Sema, maana mutumishi Wako iko anasikia." Kwa huzuni, Mungu alimwambia kijana: "Wakati umefika kwangu kwa kuazibu jamaa la Eli sawasawa na vile nilivyomwonya." Unakumbuka ni onyo gani mutu wa Mungu alikuwa amemupa Eli? (Rudilia 1 Samweli 2:29-36). Unafikiri ilikuwa vyepesi kwa Samweli kumwambia Eli kesho yake asubui yake Bwana aliyomwambia? Hapana, haikuwa vyepesi. Lakini Samweli alitoa habari kamili ya ujumbe wa Mungu.

Nyuma kidogo, sawa na vile Mungu alivyoonya, Hofuni na Finehasi waliuawa wote wawili katika vita kwa siku moja. (1 Samweli 4:11-14). Eli aliposikia habari ile, akaanguka kinyumenyume toka juu ya kiti chake – na akakufa (1 Samweli 4:18)! Mungu anachukia uasi. Halafu, Samweli akakuwa nabii wa Mungu. Alikomaa, Bwana alikuwa pamoja naye. Na watu walimusikiliza.

Katika utoto wake kule nyumbani, Samweli alikuwa kijana wa kawaida ambaye mara na mara alihitaji na kupata azabu. Kwa kadiri inavyoonekana, Hofuni na Finehasi walifanya kile walichopenda. Ambavyo viliwageukia vizuri sana?

Umekwisha kwazibiwa na wazazi wako? Umewashukuru kwa maana wanakupenda ya kutosha kwa kukuazibu? Umetambua kwamba walikupendelea wakati wanakuazibu?

Mungu anaamuru wazazi wafundishe Neno Lake kwa watoto wao. (Angalia Kumbukumbu la Torati 6:6-7; Mezali 4:1). Anawaamuru kuwaadibisha na kuwaazibu watoto wao. (Angalia Mezali 3:11-12). Maana kwa watoto kuasi wazazi wao ni zambi. Sababu Eli hakuwa mukali, wana wake hawakumutii. Halafu walikomaa hawakuweza kumutii Mungu. Na Mungu aliwaazibu kwa kifo.

Maelezo kwa mwalimu:

Wanafunzi wako wangali chini ya ulinzi wa wazazi wao? Kama ndivyo, umalize na mwito kwa ajili yao kwa kukusudia kuwa watiifu. Wamoja wanaweza kutaka musaada wa maombi wa wenzao wa somo kwa ajili ya hali ya kipekee. Kama wanafunzi wako ni wazazi, tia mukazo wa lazima ya kuwa imara, mwema, na kuwa hodari katika mafundisho ya watoto wao kwa kutii. Watu wa umri wote wanapaswa kuomba kwa ajili ya musamaha katika hali yoyote ya uasi.

SOMO 2 - UASI KATIKA TAIFA (Sehemu ya 1)

Kwa mwalimu kujifunza mbele: 1 Samweli 4:1 hadi 7:17.

Shabaa ya somo: Kuonyesha kwamba Mungu alihukumu taifa la Israeli kwa ajili ya kumuasi Yeye.
Yale ambayo wanafunzi wako wangelipaswa kujua: Kwamba Mungu ana nguvu zaidi kuliko sanamu yoyote.
Yale ambayo wanafunzi wako wangelipaswa kutambua: Kuwa na hamu kwa ajili ya inchi yao na jamii kugeuka toka miungu ya uwongo na kumutii Mungu mwenye uzima.
Yale ambayo wanafunzi wako wangelipaswa kufanya: Kuweka ushuhuda muzuri (Nyumbani, masomoni, kazini) kusudi wengine wapate kutaka kuja kwa Bwana Yesu.

Somo kwa kifupi: (kuandika ndani ya buku ya mwalimu na za wanafunzi.)
1. Waisraeli wanamuzarau Mungu. (1 Samweli 4:1-5.)
2. Waisraeli wanashindwa na Wafilistini. (1 Samweli 4:6-22).
3. Nguvu za Mungu za ajabu juu ya Dagoni. (1 Samweli 5:1 hadi 6:21.)
4. Mungu anaonyesha Wafilistini nguvu zake.(1 Samweli 7:1-17)

Shairi la kujua kwa ufahamu: "Mwogope Bwana tu, mumutumikie kweli kweli kwa mioyo yenu yote; maana kumbukeni mambo makubwa gani aliyowatendea ninyi." 1 Samweli 12:24.

Maelezo kwa mwalimu:

Kwa wakati wa somo hili Waisraeli walikuwa wakiishi katika uasi kwa Mungu. Walikuwa wameingia katika inchi Mungu aliyowaahidia. Lakini hawakutii maagizo Yake ya kuangamiza Wafilistini. Vilevile, Waisraeli waligeuka na kuabudu sanamu za kipagani. Walizarau Mungu wa kweli na Mwenye uzima. Kwa sababu hiyo walikuwa waovu kiroho na kimafikiri. Na Wafilistini walikuwa na nguvu kuliko wao. Wangelipaswa kutubu, kutafuta musamaha wa Mungu, na kumutii Yeye. Kuliko vile, walijaribu kupata majibu ya matatizo yao wao wenyewe. Matokeo yake yalikuwa hasara na kushindwa.

Angalia, tafazali, sehemu iliyotangulia ya somo hili iko mbele ya vifo vya Eli na wana wake.

Somo: Umekwisha kukusudia kufanya kitu fulani ambacho ulijua kama wazazi wako (mwalimu, ao bwana wa kazi) hawakutaka ufanye? Kulitokea nini? (Acha wanafunzi wapane mifano).

Wazazi wako walifurahi wakati uliasi? Ulisema: : Ninasikitika"? Ulisema: "Ninasikitika"? Wazazi wako walikuazibu? Waliendelea kukupernda? Katika somo letu leo, tutajifunza yale yaliyotokea wakati watu wa Israeli walimuasi Mungu. Wamoja, kama vile Samweli na wazazi wake, walitaka kumupendeza Mungu. Lakini wanaume wengi na wanawake walimuzarau Mungu na kuchagua kufuata njia yao wenyewe.

1. Waisraeli wanamuzarau Mungu (1 Samweli 4:1-5.)

Wafilistini walikuwa waadui za watu wa Mungu, Waisraeli. Waliabudu miungu ya uwongo – sanamu zilizotengenezwa na mikono yao wenyewe. Walikuwa na magari ya vita na mapanga za vyuma. Walikusudia kushinda Waisraeli na kuwafanya kuwa watumwa wao. Eli alipokuwa muzee sana, jeshi la Wafilistini lilijitayarisha kushambulia Waisraeli. Waisraeli wangelipaswa kufanya nini waliposikia hayo? (Acha wanafunzi wajibu). Wangelipaswa kuomba, wakimuuliza Mungu awambie la kufanya. Kuliko vile, wakaamua wenyewe. Wakaendelea na kwenda kupiganisha waadui zao.

Askari moja Waisraeli alianguka chini maiti. Tena mwingine … na mwingine! Waaskari Waisraeli walijikwaa juu ya wenzao waliokufa. Walilia: "Nini inatokea kwa jeshi letu? Kwa nini Mungu iko anaachilia Wafilistini watuangamize? Hatuwezi kushinda Wafilistini!" Wao, watu kweli wa pekee wa Mungu, wanapaswa kukimbia.

Wakiwa na woga, Waaskari Waisraeli walikimbia kurudi kwenye hema zao. Walilia: “Tumepoteza wanaume 4.000! Kwa nini Mungu aliacha Wafilistini watushinde? Tutafanya nini? Hatutaki kuwa watumwa wao. Tutawashinda namna gani?”

Nani angeweza kuwajibia kwa maulizo haya? (*Mungu*). Wewe ungeliwashauria kufanya nini? (*Kumwambia Eli awaombee na kutafuta musaada wa Bwana*). Lakini tena hawakumusikiliza Mungu. Kiongozi moja akaleta maoni: “Twende kwenye Hema ya Kusanyiko na tukamate Sanduku la Mungu. Tunaweza kwenda nayo katika vita pamoja nasi.” Wote wakalalamika kwa furaha: “Ndiyo, ndiyo! Tukipeleka Sanduku pamoja nasi kwa hakika tutashinda. Wakati babu zetu walipeleka Sanduku pamoja nao, Mungu aliangamiza waadui zao. Kwa hakika atafanya vilevile kwa ajili yetu!

Unakumbuka Sanduku ilikuwa nini? Ilikuwa kibweta kilichotengenezwa na muti, kilichofunikwa na zahabu. Kilikuwa karibu na urefu wa miguu mine (metre 1,125) upana wa zaidi kidogo ya miguu miwili (centimetre 60) na urefu kwenda juu wa zaidi kidogo kuliko miguu miwili (centimetre 60). Sehemu ya juu ya Sanduku, Kiti cha Rehema, ilikuwa ya zahabu nene Kiti cha Rehema ndicho kilifunika kibweta. Na kwa kila mwisho wa Kiti cha Rehema kulikuwa kerubi ya zahabu nene. Mabawa yao yalinyooka yakielekeana moja kwa lingine. Uwepo wa Bwana Mungu ulikaa katikati ya makerubi. Hii ilikuwa nafasi takatifu namna gani! Fikiri juu ya hii – utukufu wa Mungu Mwenye Uwezo ulikuwa kabisa pale kati ya Waisraeli!

Sanduku lilikuwa linalindwa katika Patakatifu pa Pakatifu, Pahali patakatifu Sana katika Hema. Hakuna mutu yeyote, isipokuwa tu Kuhani Mukubwa, ndiye aliyeruhusiwa kuingia mule. Na alipaswa kuingia mule mara moja tu kwa mwaka kwa Siku ya Upatanisho.

Sasa Waisraeli walikusudia kutosha Sanduku hiyo ya maana sana inje ya Pahali Patakatifu Sana. Walipaswa kwenda nayo katika vita! Namna gani walisubutu kufikiri kutumia Sanduku takatifu ya Mungu kama vile chombo cha kufanya muujiza? Hawakuogopa, wala kumwamini Mungu kwa kuweza kuwasaidia. Kuliko vile, wakaagiza makuhani Hofuni na Finehasi kule Shilo: “Mulete Sanduku! Mutaongoza jeshi letu kupigana na Wafilistini.”

Onyesha taswira 5: Halafu wale wana wawili wa Eli wakatii waaskari na kumuasi Mungu. Hofuni na Finehasi walipoleta Sanduku katika kambi, Waaskari walifurahi. Wakalalamika: “Twende kule na tupigane! Sasa tutashinda wale Wafilistini! Mungu aligawanya Muto Yordani wakati makuhani walipobeba Sanduku mbele ya watu. Kuta za Yeriko zilianguka wakati walibeba Sanduku kuzunguka muji. Sasa sababu tuko na Sanduku pamoja nasi, tutaangamiza Wafilistini!

2. Waisraeli wanashindwa na Wafilistini (1 Samweli 4:6-22.)

Lakini Waisraeli walikuwa wamesahau kitu kimoja. Mungu hakuwaambia wapeleke pamoja nao Sanduku kwa wakati ule, kama vile mbele. Sasa waliaminia Sanduku kuliko Mungu.

Wafilistini wakasikia makaelele na vigelegele. Wakauliza: Kunatendeka nini katika kambi ya Waisraeli? Waliposikia kwamba Waisraeli wako na Sanduku takatifu katika kambi yao, Wafilistini wakaogopa!

Walinguruma: “Sasa hatutashinda! Mukumbuke namna gani Mungu wao alishinda Wamisri? Mukumbuke namna gani walishinda wale wanaoishi hapa katika inchi hii? Tutafanya nini? Ee, tutafanya nini?”

Viongozi wao wakasema kwa sauti: “Tunapaswa tu kushinda vita hii! Tukishindwa, tutakuwa watumwa wao. Twende! Mupigane kwa nguvu yenu yote!” Wafilistini wakakimbia upande wa Waisraeli. Vita vikakuwa vikali sana. Wafilistini walilalamika: “Mukamate Sanduku! Waisraeli watajitoa wenyewe kama tunakamata Sanduku!”

Onyesha taswira 6: Vile ndivyo Wafilistini walivyofanya kabisa kabisa. Walikamata Sanduku. Waliua Hofuni, Finehasi na waaskari 30.000 Waisraeli.

Nyuma, Eli aliposikia kwamba wana wake walikufa, alianguka kinyumenyume toka kwenye kiti chake, akavunjika shingo, na kufa. Haya yote yalitendeka kwa siku moja! Unakumbuka onyo Mungu alilokuwa amemupatia Samweli? (Rudilia somo linalotangulia). Mungu anaonyesha yale Aliyosema. Na yale anayosema *yatatendeka,* yanatokea. Waisraeli walipata kujua wenyewe faida mbaya sana ya kumuasi Mungu! (Angalia Torati 28:25).

3. Nguvu za Mungu za ajabu juu ya Dagoni (1 Samweli 5:1 hadi 6:21.)

Waisraeli walirudia polepole nyumbani wameshindwa na wenye kuvunjika moyo. Lakini Wafilistini washindaji walirudi katika miji yao wakilalamika: "Tumeshinda! Tumeshinda Waisraeli! Tumekamata Sanduku! Sasa tuko na Mungu wao kwa kutusaidia!" Kwa majivuno, walikwenda kwenye hekalu lao katika muji wa Asidodi. Kule wakafanya sherehe ya ukumbusho wa ushindi wao, Sanduku, karibu na Dagoni, mungu wao aliyotengenezwa kwa mikono. Fikiri juu ya ile!

Sanduku takatifu, Sanduku yenye maana sansa ya Mungu wa kweli na Mwenye uzima, karibu na sanamu iliyotengenezwa na mikono ya watu. Dagoni alikuwa na kiwiliwili cha samaki na mikono na kichwa cha mwanadamu. Umbo gani ya kuchukiza!

Onyesha taswira 7: Kulipokuwa asubui watu waliharikisha kwenda kuangalia Sanduku – na kuabudu Dagoni. Kwa mushangao wao, Dagoni alipinduka na kulalia uso wake mbele ya Sanduku.

Watu waliuliza : "Hii ilitokea namna gani? Acha turudishe Dagoni kwa nafasi yake. Wanaume walikokotea mungu wao kwa nafasi yake ya kawaida. Asubui mapema Wafilistini wakaenda mbio kwenye hekalu. Kitisho chao, Dagoni haikuwa kwa nafasi yake. Ililala kuwa fungu mbele ya Sanduku, kichwa chake na vitanga vimevunjika! Bwana Mungu alikuwa akifundisha kwamba nguvu na heshima ni Vyake pekee. (Angalia Zaburi 96:5-8).

Haya yanatwambia nini juu ya sanamu? (Himiza wanafunzi wajibu. *Haina uzima – haina nguvu kujisaidia yenyewe. Mungu Mutakatifu wa mbinguni yuko na nguvu zote).* Mufano kamili wa Zaburi 115:3-8. Saidia wanafunzi wako kusikia kutokufaa kwa kuabudu sanamu zilizotengenezwa na watu.

Mara moja ushindi wa Wafilistini ukageuka kuwa hasara. Wale wanaoishi ndani na kandokando ya muji wa hekalu (Asidodi) walisumbuliwa na majipu makali, yenye kuuma sana. Na panya zilikuwa nafasi zote. (Angalia 1 Samweli 6:4-5).

Watu walilia: "Mapanya haya yote yanatoka wapi? Yanaharibu mashamba yetu! Tutafanya nini?" Wanaume wakakusudia: "Hatuwezi kuchunga Sanduku ya Mungu hapa. Mungu wa Israeli anatushambulia na anashambulia Dagoni, mungu wetu." Kwa mwisho wakakubali: "Tutapeleka Sanduku katika muji wa Gati."

Sanduku ilipofika Gati, maumivu ya majipu ya wanaume, vijana na wazee yakaisha palepale. Kwa hiyo watu wa Gati wakapeleka Sanduku katika muji ungine, Ekuroni. Katika Ekuroni, wengi walikufa palepale Sanduku la Mungu lilipofika. Wanaume waliobaki wazima walikuwa katika mateso ya majipu. Walilia: "Mupeleke Sanduku kule Israeli mbele tukufe sisi wote."

Wafilistini waliweza kutambua kwamba Mungu wa Israeli ndiye Mungu Mwenye Uzima. Kama kweli waliweza kumugeukia Yeye wangeliweza kuwa washindi wa jamaa la Mungu. Kuliko vile, walitaka kumuepuka. Walichagua kuendelea kuabudu mungu ambaye wao wenyewe walijitengenezea.

Kwa mwisho, Wafilistini walitgengeneza gari la kukokotwa na kupeleka Sanduku la Mungu kule Israeli. Angalia namna Waisraeli walivyofurahi kuona Sanduku linakuja nyumbani!

4. Mungu anaonyesha Wafilistini nguvu zake (1 Samweli 7:1-17.)

Pamoja na kurudia kwa Sanduku, Waisraeli waliweza kumushukuru Mungu? Waliweza kumwambia kama walisikitika maana walimuzarau Mungu? (Zungumuza). Ninahuzunika kusema, hawakufanya vile.

Walipaswa weka Sanduku la Mungu katika Hema la kusanyiko. Kuliko vile, waliipeleka kwa nyumba ya mutu moja nyumba ya (Aminadabu). Wakachagua mutu mwingine kwa kuitunza (Eleazari, mwana wa Abinadabu).Lakini sasa walionekana kusahau Sanduku. Na kama vile mataifa yanayowazunguka, waliabudu miungu ya uwongo na sanamu. Miaka ikapaita. Hawakuwa na raha. Sanamu haziwezi kusaidia wala kustarehesha watu sababu ni kazi tu ya mikono ya watu.

Miaka makumi mbili ikapita. Wafilistini waliendelea kusumbua Waisraqeli. Shauri gani ungeliweza kutolea Waisraeli? (Zungumuza). Waisraeli walikuwa wanasemezana kati yao hivi: "Ninafikiri Bwana, Mungu wetu alitusahau." Hii ilikuwa kweli? HAPANA! *Wao* ndio waliweza kumusahau Mungu!

Samweli alisikia yale walikuwa wakisema. Akauliza: "Muko na mafikiri kabisa ya kutaka kurudia kwa Bwana Mungu?" Watu wakasema kwa haraka: "Ndiyo, ndiyo." Samweli akaanza kusema: "Kama kwa kweli munataka kumugeukia Bwana, muteketeze miungu yenu yote ya uwongo. Mukusudie kutii tu Mungu Mwenye

uzima na kumwabudu Yeye peke. Mumwambie Mungu kama munahuzunika kwa ajili ya zambi zenu. Halafu mukusanyike pamoja kule Misipa na nitawaombea.

Waisraeli walirudi nyumbani na kuteketeza sanamu zao zote. Kwa kweli walitaka Mungu awasamehe. Walitaka kumwaabudu na kumutii Yeye. Unazanmi Mungu aliwasamehe? Kumbuka: Walimuasi kwa muda wa miaka mingi. Muda murefu mbele Mungu alikuwa amefanya ahadi ya ajabu sana kwa Waisraeli. Alisema hivi: "Kama kwa kweli munahuzunika kwa ajili ya zambi zenu na kuzikiri mbele Yangu, nitawasamehe." (Angalia Kumbukumbu 30:1-3; Isaya 1:18-19). Walikusanyika pamoja na Samweli kule Misipa. Hawakukula kwa siku nzima. Waliomba hivi: "Tumefanya zambi mbele Yako, Mungu wetu."

Kwa ghafula mutu moja akalalamika: "Wafilisitini wanakuja! Wafilistini wanakuja!" Waisraeli wakasihi: "Ee, Samweli, utuombee. Tutaangamizwa kama Mungu hatusaidii. Hatuko tayari kwa kupigana."

Onyesha taswira 8: Palepale Samweli akatoa mwana-kondo kama sadaka. Halafu akaomba. Na Mungu aliona kwamba watu Wake walihuzunika kwa kweli sababu ya zambi zao. Yeye ni Mungu Mwenye uzima anayesikia na kujibu maombi. (Angalia 1 Yoane 5:14-15). Unazani Bwana alijibu? (Acha wanafunzi walete mawazo).

Jemadari wa Wafilistini alilazimisha waaskari wake kwendelea mbele. Akiwa na uhakika wa kushindi, alisema bila shaka kwa sauti: "Tutaangamiza kabisa Waisraeli wote! Angalia! Hawajaribu hata kupigana!

"Pale pale kitu kisichokuwa cha kawaida sana kikatokea. (*Mwalimu:* Soma polepole 1 Samweli 7:10). Bwana akanguruma kwa sauti kubwa. Wafilistini wakaogopa na kukimbia. Waisraeli wakawafuatilia na kuwashinda. (Angalia 1 Samweli 7:11-13. Soma aya 13 polepole). Waisraeli walipata fundisho gani siku ile? (Ruhusu mazungumuzo).

Samweli akaweka jiwe kama vile alama kwa yale yaliyotendeka pale. Alikumbuka watu kadiri wote wangeweza kusikia: "Bwana ametusaidia!

Fundisho gani umepata kwa ajili yako wewe mwenyewe katika somo letu? (Pendeza kazi za kufanya kwa upekee toka somo).

1. Mungu anachukia uasi.
2. Matokeo ya kumuasi Mungu ni kushindwa, taabu, maumivu ya moyo.
3. Mungu Mwenye uzima ni mwenye nguvu zote kuliko miungu ya uwongo.
4. Sanamu hazina nguvu yoyote kwa kusaidia watu.
5. Watu hawana nguvu mbele ya Mungu Mwenye uzima.
6. Tunapokiri zambi zetu, Mungu ni mwaminifu na wa haki kwa kusamehe zambi zetu. (1 Yoane 1:9).

Ikiwa tayari umekwisha kufanya vile, unaweza kukusudia leo kumwamini Mungu Mwenye uzima? (Rudilia Hatua za Wokovu zinazokuwa kwenye ukurasa 8.)

SOMO 3 - UASI NDANI YA TAIFA (Sehemu ya 2)

Kwa mwalimu kujifunza mbele: 1 Samweli 8 hadi 12.

Shabaa ya somo: Kuonyesha kama mara kwa mara Mungu anaruhusu watu Wake wafuata njia yao wenyewe hata kama siyo mupango Wake mukamilifu kwa ajili yao.

Yale ambayo wanafunzi wako wangelipaswa kujua: Kwamba kile mutu yeyote mwingine anachofanya sicho mara kwa mara haki kwenu kufanya.

Yale ambayo wanafunzi wako wangelipaswa kutambua: Wawe na tamaa ya yaliyo bora kwa Mungu kwa ajili ya maisha yao.

Yale ambayo wanafunzi wako wangelipaswa kufanya: Wakusudie yale wanaweza kufanya juma hili kwa kutii Mungu., ndivyo kufanya mapenzi yake makamilifu.

Somo kwa kifupi: (kuandika ndani ya buku ya mwalimu na za wanafunzi.)
Wakusudie yale wanaweza kufanya juma hili kwa kutii Mungu., ndivyo kufanya mapenzi yake makamilifu.

1. Waisraeli wanaomba mufalme (1 Samweli 8.)
2. Mungu anamuchagua Saulo (1 Samweli 9 hadi 10.)
3. Saulo anashinda Waamoni (1 Samweli 11.)
4. Samweli anaonya Waisraeli (1 Samweli 12.)

Shairi la kujua kwa ufahamu: "Mwogope Bwana tu, mumutumikie kweli kweli kwa mioyo yenu yote; maana kumbukeni mambo makubwa gani aliyowatendea ninyi." 1 Samweli 12:24.

Maelezo kwa mwalimu:

Mungu anaweza kutwachilia tufuate njia yetu wenyewe hata kama siyo chaguo Lake kwetu.Utii unamuheshimisha Mungu. Uasi unatuletea huzuni! Bwana Mwenye uzima wa Waisraeli – kwa nguvu Zake mwenyewe – alishinda Wafilistini. Watu wa Mungu walipaswa kufurahia kiongozi wao. Lakini sasa wanataka mufalme, hivi wanaweza kuwa sawasawa na mataifa mengine ya kandokando yao. Ujinga gani! Mufalme mwanadamu anaweza kufanya mambo makubwa ambayo Mungu aliwafanyia? Ni ya lazima sisi kwendelea kukumbuka yale Bwana Mungu aliyetufanyia, na kumutukuza na kumushukuru!

Somo : "Watu wote wanafanya vile!"Umekwisha kusema hivyo? Je, kila mara ni vizuri na haki kuwa sawa na watu wote wengine? Waisraeli walitaka kuwa sawasawa na watu wengine. Acha tuone yale yaliyotokea.

1. Waisraeli wanaomba mufalme (1 Samweli 8.)

Siku moja, kundi la wanaume wa Waisraeli likakusanyika kwa siri. Sikiliza lile walilosema bila shaka. Musimamizi wao akasema: "Samweli anakuwa muzee. Alituongoza vizuri. Lakini sasa alituwekea wana wake watutawale kama vile Waamuzi (Viongozi). Wao si kama baba zao. Hawako waaminifu sawa vile alivyokuwa. Wanapokea rushwa toka kwa watu. Wanafanya maamuzi yasiyo ya haki."

Onyesha taswira 9: Akaongeza kusema: "Ninazani tunapaswa kuwa na mufalme kwa kututawala – sawa na mataifa mengine yanayotuzunguuka!" Wale wanaume wote wakakokota pumzi wakisema: "Mufalme?" Nyuma ya muda murefu wa kunyamaza, wakakusudia: "Labda lile ni wazo nzuri! Mataifa yote ya kandokando wako na mufalme!"

Muzee zaidi akasema kwa utulivu: "Mufalme. Mungu ndiye Mufalme wetu. Yeye Mwenyewe anatawala juu yetu. Hamukumbuki namna alivyoshinda waadui zetu, Wafilistini? (Angalia 1 Samweli 7). Mbele ya pale, aliongoza babu zetu toka Misri. (Kwa kifupi urudilie namna walivyovuka Bahari Nyekundu, Kutoka 14).

Usisahau yale Mungu aliyofanya. Alituleta katika inchi hii na kushinda wafalme wote waliokuwa wanaishi hapa. Hatuhitaji mufalme. Mufalme wetu, Bwana Mungu, ni Mwenye uwezo wote."

Lakini wengine walikataa kusikia. Walitaka mufalme *sawa na watu wengine*. Kwa mwisho wakashawishi viongozi wamwendee Samweli. Wakamwambia: "Samweli, unakuwa muzee. Na wana wako hawatuongozi katika njia sawa. Tunataka mufalme sawa na mataifa mengine."

Unafikiri Samweli alijisikia namna gani? (Alichukizwa, mwenye huzuni). Hakuwapa jibu pale pale. Alifazaika sana. Alijaribu kuwa kiongozi muzuri. Sasa Waisraeli walimukataa. Kwa hiyo akaomba Bwana.

Mungu alimufariji akisema: "Samweli, watu hawakukukataa wewe. Walinikataa Mimi kama Mufalme wao… Wamesahau yote niliyowafanyia. Kama wanakazana kuwa na mufalme, watapata taabu za kila aina." Mungu alieleza waziwazi yale yatakayofikia watu Wake kama wanapata mufalme. Halafu akaongeza kusema: "Kama watu Wangu wanahitaji kufuata njia yao wenyewe, wameweza kungojea matokeo makali."

Samweli akarudia kwenye viongozi pamoja na ujumbe wa Mungu: "Mungu aliniambia niwaonye ninyi juu ya yale mufalme atafanya. Atatuma wana wenu kwa vita. Wabinti zenu watakuwa wajakazi wa mufalme. Atatwaa mavuno yenu mazuri sana kwa matumizi yake.

Atatwaa wanyama wachaguliwa wenu kwa ajili yake mwenyewe. Mutalipa kodi ya juu. Ninyi wenyewe mutakuwa watumishi wa mufalme. Halafu mutamwomba Mungu awasaidie. Lakini Hatawajibu.

Watu wakasisitiza: "Tunataka mufalme! Tunataka kuwa sawasawa na mataifa mengine yote yanayokuwa kandokando yetu." Waisraeli walitaka kufuata njia yao wenyewe.Walikataa kusilkiliza Bwana Mungu wa mbinguni. Fikiri juu ya haya! Mungu alimwambia Samweli: " Sitaki Waisraeli wapate mufalme. Hata vilem nitawachagulia mumoja."

2. Mungu anachagua Saulo (1 Samweli 9 hadi 10.)

Nyuma ya siku chache, Mungu alimwambia Samweli siri moja. " Kesho, kwa

Wakati kama huu, nitakutumia kijana mwanaume. Atakuwa akitafuta punda za baba yake. Ni yeye ndiye nimemuchagua kuwa mufalme. Umimine mafuta juu ya kichwa chake. Umwambie kwamba atakuwa mufalme wa watu Wangu, Waisraeli."

Kwa ile siku iliyofuata, kijana moja, aliyeitwa Saulo, pamoja na mutumishi wake wakakuja kwa Samweli. Walikuwa wakitafuta punda zao zilizopotea. Lakini hawakumwambia Samweli vile.

Yule kijana Saulo, mwenye sura nzuri, hakujua siri ya Mungu. Lakini alishangaa aliposikia Samweli anasema: " Usiogope kuhushu punda zenu zilizopotea zimepatikana." Samweli aliendelea kusema: " Kuja tukule pamoja na wageni wangu na mimi. Kesho nitakwambia mambo mamoja makubwa ambayo yanalindwa kwa ajili yako." Saulo akashangaa, *mambo makubwa kwa ajili yangu? Iko anasema juu ya kitu gani?*

Kesho yake asubui mapema Samweli akaanza safari pamoja na Saulo na mutumishi wake. Samweli alimwambia Saulo: " Ambia mutumishi wako atangulie. Niko na ujumbe wako toka kwa Mungu."

<u>Onyesha taswira 10</u>: Walipokuwa wenyewe, Samweli akamimina mafuta ya muzeituni juu ya kichwa cha Saulo. Samweli akatangaza: " Mungu alikuchagua kuwa mufalme wa Waisraeli."

Saulo akafikiri: "Mimi? Mufalme wa Israeli? Niko tu kijana mulimaji. Jamaa langu halijulikani. Siwezi kuwa mufalme." Biblia inatwambia kama Saulo aligeuka kwenda nyumbani; na Mungu alibadilisha moyo wake (1 Samweli 10:9). Halafu akatambua kama Bwana atamupa uwezo wote atakaohitaji. Alikuwa tayari kuongoza na kutawala Waisraeli.

Saulo alipofika nyumbani, hakumwambia mutu yeyote yale yaliyotokea. Nyuma, Samweli aliita Waisraeli wote pamoja. Aliwakumbusha: " Mulikataa kuwa na Mungu kama vile Mufalme wenu. Munataka kuwa sawasawa na mataifa mengine yote. Kwa hiyo mutakuwa na mutawala wa kidunia. Sasa ninataka mukutane na mutu atakayekuwa nyuma kidogo mufalme wenu. Lakini mutu yule hakuonekana. Alikuwa amefichama. Watu wote waliuliza: " Yuko wapi?"

Mungu peke yake Ndiye aliyejua wapi mufalme muchaguliwa alipokuwa. Alimwambia Samweli wapi mutu yule alipokuwa anafichama. Kwa hiyo watu walimupata na kumuleta. Samweli akatangaza: Huyu ndiye Saulo, mutu Mungu aliyemuchagua kuwa siku moja mufalme wenu." Saulo alisimama murefu na mwenye sura nzuri kuliko mutu mwengine yeyote. (Angalia 1 Samweli 9:2; 10:23.)

Watu walifurahi. Wakalalamika: " Mufalme aishi maisha marefu." Nyuma wakakuwa sawasawa na mataifa mengine yote. Samweli alikuwa na mashauri fulani kwa ajili ya Waisraeli na kwa Saulo. Alianza kusema: " Munataka Mufalme kusudi mupate kuwa sawasawa na mataifa mengine. Lakini kila mufalme mutakuwa naye anapaswa kuwa *tofauti* na wafalme wa mataifa mengine. Mufalme wenu anapaswa kuwa kila mara akichaguliwa na Bwana Mungu, hapa na watu." (Angalia Toarati 17:15). Watu wote walitikisa kichwa kwa kukubali.

"Mufalme wenu anapaswa kuwa Mwisraeli, wala si mugeni hata kidogo." Watu wakasikia. "Mufalme wenu asijaribu kupitisha kiasi. Hapaswi kujitajirisha yeye mwenyewe kwa farasi, zahabu, wala feza. (Angalia Torati 17:16-17). Zaidi ya yote anaombwa kuwa na andiko sawa na Sheria ya Mungu. Anapaswa kujifunza andiko lile, kulitii, na kuogopa Bwana Mungu. Mungu ndiye Mutawala na anapaswa kuwa chini ya uongozi Wake." (Angalia Torati 17:18-20). Waisraeli wengi zaidi walifurahi kwamba siku moja, Saulo atakuwa mufalme wao. Lakini kulikuwa wafanya fujo waliomuzarau.

3. Saulo anashinda Waamoni (1 Samweli 11.)

Kisha mukutano, kila mutu akarudia kwake. Maisha yakaendelea kama kawaida. Saulo akarudilia kazi ya kulima.

Siku moja alipokuwa anarudi kutoka kwenye mashamba pamoja na ngombe dume zake, akasikia watu wa kijiji wakilia kwa sauti kubwa. Saulo akauliza: "Habari gani?"

"Waadui zetu Waamoni, wameshambulia Waisraeli wanaoishi Yabesi – Gileadi."

Wajumbe toka Yabesi-Gileadi walioleta habari hii mbaya wakaongeza kusema: "Hatutaki kupigana. Tuliomba Waamoni wafanye mapatano ya amani pamoja nasi. Walikubali, lakini kama tu tunawaacha waongoe jicho la kuume la kila Muisraeli katika muji."

"Saulo akakasirika. "Waamoni wanataka kufanya waaskari wetu kuwa wasiofaa. Mutu akiwa na jicho lake la kushoto nyuma ya ngao yake na jicho la kuume limeongolewa, hawezi kuona kwa kupigana. HAPANA! Nyinyi Waisraeli hamutapoteza macho yenu ya kuume. Tutapigana!"

Sasa Saulo alihitaji jeshi. Waaskari wa Waisraeli wanaweza kwenda kwa vita chini ya uongozi wake?

Onyesha taswira 11: Saulo akatuma wajumbe katika inchi yote ya Israeli. Kila fasi walionyesha vipande vya ngombe dume ambayo Saulo alikatakata. Mumoja akatangaza: "Huu ni ujumbe wa Saulo: Mukikataa kujiunga na jeshi letu, ngombe dume zenu zitauawa na kukatwa vipande vipande sawa na hivi." Waliposikia hivi, woga wa Bwana ukawapata Waisraeli. Na wanaume 333.000 wakageuka kwenda kupigana.

Kesho yake asubui mapema, Saulo na jeshi lake walifanya shambulizi la kushangaza. Waliingia katika kambi ya adui na kushinda kabisa kabisa Waamoni! Waisraeli walifurahi na yale Saulo aliyofanya. Wakalalamika hivi: "Mufalme aishi maisha marefu! Mufalme aishi maisha marefu! Ametuongoza kwenye ushindi juu ya waadui zetu. Tutamuua yeyote anayepinga Saulo!"

Saulo akasema kwa sauti: "Hakuna mutu atakayeuawa! Sikupata ushindi. Bwana ndiye ametuokoa toka waadui zetu!" Halafu Samweli aliwaambia watu hivi: "Mukuje! Tutakwenda Giligali. Kule tutatangaza mbele ya Bwana kama Saulo ndiye mufalme wetu." Halafu wote walienda na kufanya sherehe kubwa. Munazani Waisraeli walikuwa na haki kwa kuchagua Saulo? (Muwe na mazungumuzo. Inaonekana kama walikuwa nayo. Lakini ni haki kuendelea kukataa yale Mungu anataka? Soma Isaya 40:21-24, 28-31. – Onyesha kwamba Mungu ndiye mwenye nguvu kila wakati – mwenye uwezo wote. Umbalimbali na ile, soma Isaya 40:6-8, inayosema juu ya wanadamu, na Saulo vilevile. Ni Mungu ao Saulo ndiye angekuwa mufalme muzuri zaidi?).

4. Samweli anaonya Waisraeli (1 Samweli 12.)

Samweli alikuwa sasa muzee. Alijua ilikuwa wakati wa kuacha kazi yake kama vile mwamuzi wa Waisraeli. Alitumikia Mungu kwa imani kama vile kiongozi wao kwa miaka mingi. Aliendelea na kazi yake ya ukuhani na nabii. Tangia pale Saulo alikuwa mufalme na kiongozi wao.

Samweli akakusanya pamoja watu wa Israeli. Akasema: " Mumechagua mufalme kwa kuwatawala. Lakini musimusahau Bwana Mungu wenu. Kila wakati babu zetu walikosa kutii amri Zake, Aliwaazibu. Mukikosa

kumutii Bwana, na mukimuasi, atawaazibu ninyi. Lakini mukimuheshimu Bwana Mungu, mukimutii na kushika amri zake, atawabariki ninyi na mufalme wenu." Watu wote wakakubali.

Onyesha taswira 12: Lakini kicheko chao kilitoweka wakati Samweli aliendelea kusema: "Mulifanya makosa mulipoomba mufalme. Munajua mvua hainyeshi kwa wakati huu wa mwaka wakati munavuna ngano. Lakini nitaomba Bwana kutuma umande wa mvua. Halafu mutajua ulikuwa uovu wa namna gani kwenu kwa kuomba mufalme."

Halafu Samweli akaomba Bwana. Na kwa siku ile ile Mungu akanyesha umande wa mavua. Ee, mvua ya namna gani! Mara moja Waisraeli wakatambua kama kwa kwomba mufalme, walimukosea Mungu. Wakasihi hivi: " Samweli, utuombee. Kama hautuombei, tutakufa!"

Samweli akahakikisha tena watu akisema: " Mungu anaendelea kuwapenda. Hatawaachilia. Ninyi ni watu wake wa kipekee ambao alichagua kwa ajili Yake Mwenyewe. Lakini mukumbuke, sanamu isiyofaa haiwezi kuwasaidia. Mungu wetu wa mbinguni, Yule anayeishi na mwenye nguvu ndiye anayesikia na kujibu maombi. Mumukumbuke Yeye. Mumutumikie kwa moyo wenu wote. Mutii maagizo yake yote. Musiogope. " Soma 1 Samweli 12:24-25). Ni Mungu gani wa neema na mwenye kusamehe Waisraeli walimutumikia! Na ni Mungu wetu – Yule tunayemutumikia leo. Tuseme kwa pamoja aya yetu ya kujua kwa ufahamu. (1 Samweli 12:24).

Samweli alikumbusha Waisraeli kwamba Mungu alitangulia kuwaongoza toka utumwa katika Misri. Aliwalinda na kuwapa ushindi juu ya waadui zao. (Mwalimu : Somea wanafunzi wako polepole Waroma 8:32. Mungu alitufanyia nini? *(Alitoa Mwana Wake wa pekee kufa juu ya musalaba kwa ajili yetu sisi tunaokuwa watumwa wa zambi).* Umekwisha kukubali zawadi kubwa ya wokovu ya Mungu? Bwama Yesu Kristo ndiye Mufalme wa maisha yako?

Wakati Mungu amekufanyia mengi kama na haya madaraka yako ni gani Kwake? *(" Umutumikie kwa kweli kwa moyo wako wote.")* Unaweza kumutumikia namna gani? (Acha wanafunzi wazungumuzie yale wanaweza kufanya kwa ajili ya Bwana leo na katika juma linalokuja. Kila moja aandike kusudio lake katika buku lake.

SOMO 4 – UASI WA MUFALME

Kwa mwalimu kujifunza mbele: 1 Samweli 13:1 hadi 15:35

Shabaa ya somo: Kuonyesha kwamba kutokutii na uasi vinaweza kuleta musiba, taabu na kukataliwa.
Yale ambayo wanafunzi wako wangelipaswa kujua: Mungu anaona kila kitu tunachofanya; hakuna zambi inayofichama mbele Yake.
Yale ambayo wanafunzi wako wangelipaswa kutambua: Kuwa na hamu ya kuwa wenye haki kila mara na katika kila hali.
Yale ambayo wanafunzi wako wangelipaswa kufanya: Kusema kweli kila mara, kutii mwenye mamlaka, kuheshimu Bwana kwa midomo yao na katika maisha yao.

Somo kwa kifupi: (kuandika ndani ya buku ya mwalimu na za wanafunzi.)
1. Kutovumilia kwa Mufalme Saulo. (1 Samweli 13:1-23.)
2. Uongozi wa kipumbafu wa Saulo.(1 Samweli 14:1-52.)
3. Utiifu wa nusunusu wa Saulo. (1 Samweli 15:1-21.)
4. Mungu anamukataa Mufalme Saulo. (1 Samweli 15:22-35.)

Shairi la kujua kwa ufahamu: "Mwogope Bwana tu, mumutumikie kweli kweli kwa mioyo yenu yote; maana kumbukeni mambo makubwa gani aliyowatendea ninyi." 1 Samweli 12:24.

Maelezo kwa mwalimu:

Mbele ya kufanya utangulizi wa somo hili, uwape wanafunzi wakati wa kueleza furaha wanayokuwa nayo kwa kumutumikia Bwana tangia somo lililotangulia.

Kwenda mbali na Mungu ni huruma sana. Zambi inaota na palepale maisha yanabadilika. Na mutu anayefuata njia yake mwenyewe kuliko njia ya Mungu, anaingia zaidi na zaidi ndani ya zambi. Mwisho wake ni uharibifu. (Mezali 16:25). Saulo alijua Mungu alimwamuru afanye nini. Ingawa hivyo, polepole moyo wake ulianza kupoa juu ya Bwana. Zambi moja inaongoza kwenye ingine. Kutenda mabaya kunakuwa kwepesi. Anavutwa tu na yeye mwenyewe. Kwa vile alivyomwacha Mungu, na kushuka mbio zaidi katika njia pana kwenye uharibifu. Ni hivi itakavyokuwa na yeyote anayechagua kufuata njia yake mwenyewe.

Somo: Utii ni moja kati ya mafundisho magumu ya somo letu. Sisi wote tunataka kila moja kufuata njia yake mwenyewe. Lakini kumbuka: Tunaweza kuchagua kutomutii Mungu, lakini hatuwezi kubadilisha matokeo ya yale tuliyochagua! (Rudilia kwa kifupi maarifa ya Adamu na Eva katika shamba).

1. Kutovumilia kwa mufalme Saulo (1 Samweli 13:1-23.)

Mambo yaliendekea Waisraeli vibaya. Waisraeli walijua kama Wafilistini walikuwa wakikusanya tena jeshi kubwa. Walikuwa na magari 3.000, waaskari wapanda farasi 6.000, na waaskari zaidi wasioweza kuhesabiwa.

Mufalme Saulo akaogopa. Alikuwa amechagua tu Waaskari 3.000 (1 Samweli 13:2). Namna gani angeliendelea kushinda Wafilistini na jeshi ndogo kama hili? Nani angeliweza kumupatia mufalme uwezo wa kushinda? *(Mungu)*. Zamani, Samweli alikuwa amemwambia Mufalme Saulo kwenda Giligali. Aliamuru: " Saulo, uningojee kule muda wa siku saba. Nitakukutana Giligali.

Nitakapokwisha kutoa sadaka kwa Mungu, nitakwambia utakachofanya." (Angalia 1 Samweli 10:8). Kwa hiyo mufalme Saulo alingojea. Lakini Wafilistini walikuwa wanasogelea karibu sana. Jeshi lao liliongezeka kwa hesabu. Waaskari wa Saulo waliogopa sana. Walifichama ndani ya mashimo na matundu na miamba.

Wamoja walilia hivi: " Hatutaweza hata kidogo kushinda Wafilistini. Hatuna hata gari moja, wala mapanga, wala mishale. (1 Samweli 13:19-21). Namna gani tunaweza kuwashinda? Tutaangamizwa!"

Kufuatana na ile, jeshi la Saulo likakuwa na waaskari wachache sana kuliko mbele. Wale walibaki walitetemeka kwa woga. Mumoja akauliza: " Kwa nini Mufalme Saulo hatuongozi katika vita? Iko anangojea nini?

Saulo alipaswa kutia waaskari wake moyo kwa kukumbusha yale Mungu aliyofanya kwa ajili yao kule Yabesi-Gileadi. (Acha wanafunzi waseme matokeo toka somo No. 3; 1 Samweli 11) Saulo angeweza kukumbuka yeye mwenyewe kwamba Mungu alipata ushindi ule. Alipaswa kukumbuka umande na mvua kubwa Mungu alivyotuma kwa kuonyesha kwamba ombi lao kwa kupata mufalme halikumupendeza Yeye.

Alipaswa kuhakikishia waaskari wake kama Samweli anapaswa kuja kuwaambia la kufanya. Kuliko vile, Saulo alikuwa akienda na kurudi mbele ya hema yake. Alifikiri: "Hii ndiyo siku ya saba. Samweli hajafika bado hapa. Waaskari wangu wanaanza kunikimbia. Nitafanya nini?"

Kiongozi moja akauliza: "Mufalme Saulo, mupaka wakati gani tutaendelea kungojea? Waaskari wetu wako wanakimbia. Hauwezi kupiganisha Wafilistini bila jeshi." Saulo akajibu: "Unasema kweli! Lakini hatuwezi kupigana mpaka tunatoa sadaka kwa Mungu. Kwa sababu Samweli hajafika bado, muniletee wanyama wale."

<u>Onyesha taswira 13</u>: Basi Saulo akatayarisha sadaka, akaiteketeza, na kuomba. Akatangaza hivi: "Sasa tunapaswa kupigana. Hatutaendelea kungojea." Je, Mufalme Saulo alifanya mambo ya haki? (Acha wanafunzi wazungumuze. Saulo alikuwa akiasi Mungu kwa makusudi. Ni makuhani tu ndio walipaswa kutoa sadaka. Samweli, kuhani wa Mungu alikuwa amesema: "Ngoja." Kuliko kungojea, Saulo alifanya yale alitaka kufanya.

Kwa wakati ule, Samweli akafika. Alipoona sadaka yenye kuteketezwa, akauliza: "Saulo, ulifanya nini?" (Wanafunzi wasome 1 Samweli 13:11-12). Saulo akajibu: "Kwa kweli hauwezi kunikaripia kwa yale niliyofanya. Ni nini tena ningeliweza kufanya?" Alikuwa akisema kweli? Unafikiri Mungu angeliweza kumusamehe Saulo kama angeliweza kukiri zambi yake na kwomba musamaha? (*Bila shaka*. Mifano: 1 Samweli 7:2-10; 12:19-25).

Saulo alikuwa na kiburi sana kwa kuomba Mungu amusamehe. Samweli akamuambia kwa huzuni: "Saulo, ulikuwa mujinga sana. Unajua kama ni kuhani tu ndiye anapaswa kutoa sadaka. Ulimuasi Bwana Mungu. Mungu alipanga kwa ajili yako na wana wako kutawala watu wa Israeli nyuma yako. Lakini sababu ulimuasi Yeye, sasa Alichagua mutu mwingine kuwa mufalme." Halafu Samweli akageuka na kwenda zake.

2. Uongozi wa upumbafu wa Saulo (1 Samweli 14:1-52.)

Kwa huzuni Mufalme Saulo alirudia nyuma na waaskari 600 tu. Alikuwa amevunjika moyo. Aliogopa. Kiongozi maskini namna gani! Moja kati ya waaskari wa Saulo alikuwa mwana wake, Yonatana. Alikuwa tofauti na baba yake. Alimwamini Bwana Mungu. Alikuwa hodari Aliomba Mungu apate kumwongoza.

Siku moja Yonatana alipata wazo moja. Akamugeukia yule aliyekuwa akimubebea silaha. Yonatana akanongoneza hivi: "Wafilistini wamoja wanapiga kambi katika bonde juu ya jiwe lile kubwa: Kuja! Wewe pamoja nami twende juu na kuwashambulia Bwana Mungu hahitaji jeshi kubwa kwa kushinda waadui zetu. Anaweza kufanya vile kwa vyepesi na wawili!"

Mubebeaji wa silaha akajibu: "Yonatana, niko tayari kufanya chochote unachosema. Yonatana akaonya: "Tunataka kuwa na uhakika kama haya ni mapenzi ya Mungu." (*Mwalimu:* Soma kwa sauti 1 Samweli 14:8-10). Wafilistini walimwona Yonatana na mubebeaji wake wa silaha wakivuka katikati yao. Wakalalamika; "Mupande huku!" Yonatana akanongonezea mubebeaji wake wa silaha hivi: "Unifuate! Bwana ameweka Wafilistini katika mikono ya Waisraeli." Wote wawili wakapanda juu ya kambi ya jeshi na palepale wakaua waaskari 20. Kisha udongo ukatetemeka. Wafilistini wakaogopa!

Walinzi wa Mufalamue Saulo walikuwa wakiangalia tokea kwa mbali. Walipoona Wafilistini wakisambaa katika pande zote, wakamwelezea mufalme. Saulo akasema kwa sauti: "Ni nani anayewashambulia? Ni nani asiyekuwa katika kambi yetu? Jibu likakuja: "Yonatana pamoja na mubebeaji wake wa silaha hawako hapa!" Kwa haraka Saulo akakusanya waaskari wake kwa kujiunga katika vita.

Saulo akaamuru: "Munisikilize! Yeyote atakayekula kitu chochote leo atalaaniwa. Kutokula kabisa kitu chochote mupaka nitakapopata ushindi juu ya waadui zangu." Kwa nini Saulo alipana agizo la kijinga kama

hili*? (Alitaka kupata sifa njema kwa kushinda Wafilistini. Alitaka wengine waone kama yeye, mufalme, anatawala)*

Yonatana hakusikia agizo la baba yake. Alivyokuwa anafukuza Wafilistini katika pori, akaona asali. Akachovya muti ndani ya sega la asali na kulamubula asali. Palepale akapata nguvu na kuendelea kupigana . Lakini waaskari wengine waliteswa sana na njaa. Wakakuwa wazaifu sana hata hawakuweza kushinda Wafilistini.

Nyuma, Yonatana halisikia agizo la kijinga la baba yake. Akawaambia waaskari: " Si muujiza kwamba hamukukuwa na nguvu za kutosha kwa kupigana. Kama tu mungelikula asali kidogo, tungeliweza kupata ushindi mukubwa leo. Baba yangu ndiye ameleta taabu." Saulo alikasirika sana alipasikia kwamba Yonatana alikosa kutii amri yake.

Akaisha kutoa ahadi, basi akasema: "Yonatana, mwana wangu, unapaswa kufa!"

Onyesha taswira 14: Waaskari wakasema kwa sauti: "Hapana, hatakufa. Yeye ndiye Mungu alitumia kwa kupata ushindi wa leo. Hakuna unywele moja wa kichwa chake utakaoanguka juu ya udongo!" Kwa haraka waaskari wakamwokoa Yonatana. Watu wamoja waliotia mukazo kwa kupata mufalme, sasa walikuwa wapinzani wake. Saulo alinyenyekezwa mbele ya jeshi lake. Kwa nini? Sababu alichagua kufanya yale aliyotaka kuliko kuomba uongozi wa Mungu.

Bwana aliwaonya watu kwamba mufalme wao latakuwa sultani (mugandamizaji). (Angalia 1 Samweli 8:9-18) Na huu ulikuwa mwanzo.

3. Utiifu wa nusunusu wa Saulo (1 Samweli 15:1-21.)

Siku moja Samweli akamwendea Saulo na ujumbe toka kwa Mungu. Alisema hivi: "Unisikilize vizuri. Waamaleki ni wabaya. Watu wetu walipokuwa wanarudi kuelekea Kanana, Waameleki walifanya ushambulizi wa kinyama juu ya wazee, wanawake na watoto waliobaki nyuma. (Angalia Torati 25:17-19; Kutoka 17:1-16) Mungu alisema tunapaswa kuwaazibu tutakapopata inchi. Amri yake ilipaswa kutiishwa tangia zamani. Sasa, Mufalme Saulo, ongoza jeshi lako kwa kuwashambulia Waamaleki. Uwateketeze *wote* – mufalme wao, wanaume, wanawake, na watoto. Usiache *kitu chochote*!"

Amri ya Mungu ilikuwa wazi? (*Ndiyo*! Kumbusha wanafunzi juu ya ahadi ya Mungu katika Mwanzo 12:3. Kabila la Amaleki lililaani Israeli).

Akitii amri ya Mungu Saulo alikusanya jeshi lake. Akasema kwa sauti: "Mushambulie!" Kwa haraka yeye na waaskari wake wakashinda kabisa kabisa Waamaleki.

Onyesha taswira 15: Waaskari wakachunguza kondoo na wanyama wengine. Askari moja akauliza: " Mufalme unazani kwa kweli tunapaswa kuwaua wote? Tunaweza kuchunga wamoja kati ya walio wazuri?"

Saulo angepaswa kujibu nini? (Acha wanafunzi wajibie). Angelipaswa kusema hivi kwa sauti: " HAPANA!" Kuliko kujibu vile, alijibu hivi: "Ninazani itaweza kuwa vizuri kwacha wanyama wazuri zaidi. Lakini mwuue wengine!"

Ubaya uko wapi katika jibu lake? (Aliasi amri ya Mungu).

Saulo akauliza waaskari: "Watu wote wameuawa?" Waaskari nao wakauliza: "Ndiyo wote, isipokuwa mufalme ambaye umemukamata. Unataka tumuue sasa hivi?"

Saulo akasema: "Hapana."

Kosa lilikuwa gani katika uamuzi wa Saulo? (Aliasi Mungu bila kusukumwa.)

Saulo alifurahi sana na ushindi wake hata akajenga munara kwa kujiheshimisha yeye mwenyewe (1 Samweli 15:12). Lakini ingawa vile Saulo alijisifu yeye mwenyewe, nani aliyemukasirikia? (*Mungu* 1 Samweli 15:11).

Mungu akamwambia Samweli: "Ninahuzunika kwamba Saulo alikataa kunitii Mimi. Sitaendelea kumutumikisha kama mufalme juu ya watu Wangu."

Samweli alipomwendea Saulo, Saulo akamusalimia kwa furaha. "Samweli, nimetii amri ya Bwana." Samweli akajibu: "Ninasikia sauti ya kondoo wenye kulia, na mulio wa ngombe. Hii ina maana gani?"

Saulo akajibu hivi: "Waaskari waliacha wanyama wazuri sana. Tutawatoa sadaka kwa Bwana Mungu wako. Lakini tuliteketeza kila kitu kingine."

4. Mungu anamukataa mufalme Saulo (1 Samweli 15:22-35.)

Kwa huzuni Samweli alisema: “Saulo kwa nini ulikataa kutii Bwana Mungu? Kwa nini ulimuasi na kutenda mabaya mbele ya macho Yake? Mungu hataki sadaka zako. Anataka utii! Saulo, sababu umekataa neno la Bwana, Naye amekukataa wewe kama vile mufalme wa Waisraeli.”

Saulo akashituka. “Nimefanya zambi. Nimesikiliza watu kuliko Mungu. Tafazali unisamehe na wende kuabudu Bwana pamoja nami.”

Samweli akasema kwa nguvu: “Saulo, kweli hapana. Sitakwenda pamoja nawe. Sababu ulikataa kumutii Mungu, alikwisha kukukataa kama mufalme wa Israeli!”

Saulo alikata tumaini. Alivyokuwa anamushika Samweli kwa kutaka kumuzuia asiende, Saulo akapasua kanzu ya Samweli.

Onyesha taswira 16: Akiwa anamugeukia Saulo, Samweli akasema: “Sawasawa na vile umepasua kanzu yangu, ndivyo Mungu amepasua toka kwako Ufalme wa Israeli. Amekwisha kupatia mutu mwingine anayekuwa bora kuliko wewe. Hii ndiye mwisho. Mungu anatimiza yale anayosema.”

Saulo akapata wazimu. Akasihi hivi: “Tafazali, tafazali unisamehe. Nimekosa. Lakini kuja na uabudu pamoja nami na uniheshimishe mbele ya watu.”

Samweli akaenda na Saulo. Samweli akauliza: “Muniletee Mufalme Agagi. Nitawaonyesha namna gani Mungu anachukia uovu wa mufalme huyu mubaya.” Samweli akauwa Agagi, Mufalme Saulo akiwa anaona, na akiwa mwenye kuogopa.

Maisha ya Saulo yaliendelea na kushuka. Alipofanya zambi na kuibeba, alijisamehe yeye mwenyewe. Kwa hiyo Saulo akakuwa mubaya zaidi na mwenye taabu mupaka siku alipokufa. Kama hadisi ya maisha *yako* ingeliweza kuelezwa, nini ingelisemwa juu yako? Kama vile Saulo, ulikataa kumutii Mungu na Neno lake? Sikiliza vizuri yale Bwana anayosema.

(Mwalimu: Maliza kwa heshima kwa kusoma Maandiko, sjairi zinazoweza kutumiwa kwa kundi lako. Kwa mufano, kama uko unafundisha *watoto*, unaweza kutumia Waefeso 6:1-3; Wakolosayi 3:20.

Vijana: 1 Petro 5:5; 1 Timoteo 4:12.
Wanawake : Waefeso 5:22-28; 1 Petro 3:1-6
Wanaume : Waefeso 5:25, 28; 1 Petro 3:7
Wafanya kazi : Waefeso 6:5-8; Wakolosayi 3:22-25; 1 Timoteo 6:1; 1 Petro 2:18-20
Wakubwa wa kazi : Wakolosayi 4:1.
Wasiokoka : 2 Watesalonika 1:7-9; 1 Petro 4:17.
Waamini : Waebrania 13:17

Haya ni maagizo ya maana ya Bwana Mungu ya kuweza kutii. Kumbuka: Wale wanaokataa kutii Mungu na Neno Lake wanapaswa kupata matokeo yake. Maana kila mara Mungu anaazibu wale wanaofanya zambi.

****

KULETA MUTU KWA MWOKOZI

MANENO YA KWELI YA KUONYESHA WAZI KATIKA SOMO :

1. Bwana Yesu ni Mwana wa Mungu
2. Bwana Yesu alikuja duniani kwa kufa. Kalvari haikuwa kosa; haikuwa musiba. Ilipangwa mbele dunia ipate kuumbwa
3. Mungu ni mwenye haki. Alisema ataazibu zambi kwa njia ya kifo; Anapaswa kutimiza Neno Lake. Bwana Yesu alikuwa tayari kubeba azabu kwa kufa juu ya musalaba kwa ajili ya zambi *zetu.*
4. Yesu hakufa sababu *alipaswa*. Alikufa sababu alitupenda sana hata *akataka*
5. Tunapokubali kifo cha Kristo kama vile malipo kwa ajili ya zambi zetu, hatutaweza tena kuazibiwa kwa ajili ya zambi ile. Mungu ni mwenye haki na hawezi kuazibu zambi mara mbili.

MANENO YA KWELI YA KUONYESHA WAZI WAKATI WA MATENGENEZO

1. Mungu ni Mutakatifu, Mwema na Mwenye upendo. Hakuna zambi inayoweza kuwa mbele yake.
2. Umbalimbali na Mungu, sisi ni wenye zambi. Mioyo yetu ni midanganyifu na miovu. Kila mutu katika dunia yote amefanya zambi na kupungukiwa na utukufu wa Mungu. (Angalia Waroma 3:23).
3. Zambi inapaswa kuazibiwa. Hatuwezi kujiokoa wenyewe toka zambi yetu. Mushahara wa zambi ni mauti (Waroma 6:23). Mungu anapaswa kutimiza Neno Lake.
4. Bwana Yesu Kristo, Mwana wa Mungu, alipata azabu kwa ajili yetu na kufa kwa nafasi yetu. (Angalia 1 Petro 2:24).
5. Kwa uamuzi wetu wenyewe, tunaweza kuamini haya na kumupokea Bwana Yesu kama vile Mwokozi wetu. Tunaweza kusema " Ndiyo" ao "hapana." Mungu alituumba kwa namna hiyo. (Angalia Yoane 3:18),
6. Tunapomupokea anatupatia zawadi ya ajabu, zawadi ya uzima wa milele. (Angalia Yoane 3:16). Na kwa wakati uleule anatupatia Roho Mutakatifu kukaa ndani yetu kwa kutusaidia.
7. Tunaweza kujua kwa mara moja toka Neno la Mungu kama tumezaliwa kwa mara ya pili na kama zambi zetu zimesamehewa. (Angalia 1 Yoane 5:11,12).
8. Kisha kumupokea Bwana Yesu, na tunapofanya kosa; tunapaswa mara lmoja kumwomba atusamehe. (Angalia 1 Yoane 1:9). Kama kwa kweli tunahuzunika sababu ya kosa tulilofanya, atatusamehe. (Sababu Anajua mioyo yetu, Anajua kweli kama tunahuzunika. Anajua kama tunakusudia ndani ya mioyo yetu kama hatutafanya zambi tena). Kama tunamwomba, Atatusaidia kufanya yale yanayomupendeza.
9. Mungu anataka watoto wake wakomae (Angalia 2 Petro 3:18). Tunakomaa (1) Kwa kusoma Biblia, (2) Kwa kumwomba, (3) kwa kwenda kwa nyumba Yake kwa kuabudu, na (4) kwa kuwaelezea wengine juu Yake.

UNAPOONGOZA ROHO KWA KRISTO, KILA MARA UINGIZE HATUA HIZI TANO:

1. Umwonyeshe HITAJI lake la Mwokozi – wote ni wenye zambi. (Angalia Waroma 3:23)
2. Umwongoze katika NJIA ya wokovu : Bwana Yesu Kristo (Isaya 53:6)
3. Umwalike KUPOKEA Bwana Yesu kama vile Mwokozi (Yoane 1:12).
4. Umwonyeshe aya ya UHAKIKA kwamba anapaswa kutangaza kwa ajili yake mwenyewe (Yoane 3:36; 5:24).
5. Umusukume katika KUKOMAA. (2 Petro 3:18).

SAIDIA MUTOTO ALIYEKIRI BWANA YESU KUKUMBUKA MANENO HAYA YA KWELI:

(Uwalinganishie na Yoane 3:16).

1. Mungu ananipenda.
2. Nimnefanya zambi.
3. Kristo alikufa kwa ajili yangu.
4. Nimemupokea.
5. Sasa nina uzima wa milele.